# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Kwa mujibu wa uwezo aliopewa chini ya Kifungu Namba 53 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi amemteua **Bwana Suleiman Ahmed Salum** kuwa **KATIBU WA RAIS.**

Kabla ya Uteuzi huo, Bwana Suleiman Ahmed Salum alikuwa Mkurugenzi Msaidizi katika Tume ya Pamoja ya Fedha Tanzania.

Aidha, kwa mujibu wa uwezo aliopewa chini ya Kifungu Namba 6(1) cha Sheria ya Shirika la Bandari Namba 1 ya mwaka 1997, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi amemteua **Bwana Nahaat Mohammed Mahfoudh** kuwa **MKURUGENZI MKUU WA SHIRIKA LA BANDARI, ZANZIBAR.**

Kabla ya Uteuzi huo Bwana Nahaat Mohammed Mahfoudh amefanyakazi katika Taasisi mbali mbali za sekta binafsi.

Uteuzi huo umeanza leo tarehe 04 Novemba, 2020.

**(Dkt. Abdulhamid Y. Mzee)**
**KATIBU WA BARAZA LA MAPINDUZI**
**NA KATIBU MKUU KIONGOZI,**
**ZANZIBAR.**

**04 NOVEMBA, 2020**